



### **Tanzania Human Rights Defenders Coalition [THRDC-Coalition]**

P. O. Box 75254 Dar es Salaam, TANZANIA Telephone: +255-22-2773038/48, Fax: +255-22-2773037, Mob: +255 783 172394 E-mail: [defenderscoalition@rocketmail.com](mailto:defenderscoalition@rocketmail.com)

## **TAMKO KWA UMMA KULAANI VURUGU ZILIZOTOKEA KATIKA MDAHALO WA KATIBA INAYOPENDEKEZWA TAREHE 2/11/2014 JIJINI DAR ES SALAAM**

Mtandao wa Watezi wa Haki za Binadamu (THRDC) umesikitishwa na kitendo cha kudhalilisha kilichofanywa na kundi la watu wachache wanaodaiwa kuwa na maslahi ya chama kwa ajili ya kuvuruga mdahalo wa kujadili katiba inayopendekezwa ulioandaliwa na Taasisi ya Mwalimu Nyerere katika ukumbi wa Ubungo Plaza tarehe 2/11/2014.

Mtandao unakemea vikali kitendo hicho kilicho watia hatarini watetezi wa haki za binadamu, wahandishi wa habari pamoja na wahudhuriaji wengine kwani kililelnga kuvunja amani ya eneo lile. Vurugu hizo zingeweza kusababisha maafa makubwa kwa watu na mali endapo kundi kubwa la wananchi waliohudhuria mdahalo huo wangeamua kupambana na hilo genge la wahuni lilotumwa na kundi fulani la wanasiasa kuharibu mdahalo huo.

Pia mtandao unalaani vikali kitendo cha kuvamiwa kwa wasemaji wa mdahalo huo akiwemo Jaji Warioba. Kitendo hicho kimewadhalilisha sio tu watoa mada bali watanzania wote kwa ujumla na kuvunja haki ya kutoa maoni na kujumuika.

Kutokana na vurugu hizo watu hao wamevunja Ibara ya 18, 20 na 26 za katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzuia uhuru wa kutoa maoni, uhuru wa kushirikiana na wengine na pia wameshindwa kutekeleza wajibu wa kutii sheria za nchi. Hivyo basi kwa makosa hayo tunaisihi serikali kutolifumbia swala hili macho na ihakikishe watuhumiwa wanafikishwa kwenye mikono ya sheria.

Suala la Katiba ni suala la Kitaifa na wala si suala la kikundi kimoja, hivyo kitendo chochote cha kutaka kuwanyamazisha watanzania wasiseme lolote kuhusu katiba pendekezwa ni dalili za kutaka kuipelekeea nchi kwenye machafuko. Wananchi ama kundi lolote la kijamii lina haki kuendesha

---

Board of Directors:

Dr. Helen Kijo Bisimba, Kharous Mpatani, Martina Kabisama, Tike Mwaipabipile, Joseph Parsambei, Saed Kubenea, Hamisa Mmanga and Ernest Kimaya.

midahalo na kuelimishana kuhusu Katiba pendekewza kwa kuangalia kama imekidhi matarajio ya Watanzania.

Ikumbukwe kuwa, katika karne hii Tanzania inatakiwa kutengeneza Katiba itakayokua ya mfano ulimwenguni kwani nchi sasa haipo kwenye mfumo wa chama kimoja kama ilivyotengenezwa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Vilevile Mtandao unalaani vikali matukio yanayoendelea kuwatishia waliokua wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba (BMK) kutoka upande wa Zanzibar waliopiga kura ya wazi ya HAPANA.

Matukio hayo ya vitisho kwa Bw. Adil Mojammed na Bi. Salma Said ni pamoja na kufuatiliwa na vijana wanaoaminika kutoka kweye kundi la kisiasa huku wakiwashutumu kuwa wamemdhalilisha Rais wa Zanzibar.

## **WITO WETU**

- Asasi za kijamii kuwa na umoja na mshikamano ili kuweza kuwa na sauti ya pamoja katika hatua zote za Mchakato wa Katiba zilizobaki,
- Asasi za kiraia kujali suala la ulinzi na usalama hasa wakati huu wa mchakato wa kupata katiba mpya.
- Wanasiasa kujali maoni ya watu na kuheshimu mitazamo ya wengine kipingana kwa hoja na si kwa kuandaa vikundi vya wahuni kuvuruga mijadala ya kitaifa.
- Wadau wa maendeleo waone uhitaji wa kuzisaidia asasi za kiraia katika suala la katiba ili ziweze kupaza sauti ya pamoja katika hatua zinazofuata za mchakato wa katiba.
- Mtandao unaishauri jamii na hasa vijana kuwa mfano wa kuigwa na kuepuka kutumiwa na watu wachache wenyе maslahi yao ya kutaka kuifanya nchi isipate katiba ya kweli.
- Vyombo vya usalama kuhakikisha kipindi hiki wanakuwa makini sio tu kwa mikutano ya nje bali hata mikutano ya ndani ili kuepuka umwagaji wa damu.
- Viongozi wa Dini wakemee kwa nguvu zao zote chama chochote kile kinachoondaa wahuni kwa ajili ya kuvamia midahalo ya kiraia kuhusu mchakato wa Katiba mpya.
- Tunawasihi wananch wote , makundi ya kijamii na AZAKI kukemea tukio hili la jana kwani ishara mbaya kwa amani ya Taifa.

---

Board of Directors:

Dr. Helen Kijo Bisimba, Kharous Mpatani, Martina Kabisama, Tike Mwaipabipile, Joseph Parsambei, Saed Kubenea, Hamisa Mmanga and Ernest Kimaya.

**Mungu Ibariki Tanzania Bara,**

**IMETOLEWA NA MTANDAO WA WATETEZI WA WA HAKI ZA BINADAMU TANZANIA**



---

Board of Directors:

Dr. Helen Kijo Bisimba, Kharous Mpatani, Martina Kabisama, Tike Mwaipabipile, Joseph Parsambei,  
Saed Kubenea, Hamisa Mmanga and Ernest Kimaya.